

A SHERIA NA AHADI. Wagalatia 3:21.

- ❖ Imani na sheria vinamajukumu tofauti katika mpango wa wokovu.
- ❖ Mafarisayo walifikiri sharia ingeleta uzima kwasababu iliandikwa kwamba mwanadamu “ataishi kwa hizo” (Walawi 18:5). Lakini sheria haiwezi kuleta uzima wa kiroho, kwani ni Mungu pekee awezaye kufanya hivyo kupitia Kristo.
- ❖ Ndio maana Paulo alielezea kazi ya sharia katika maisha yetu.

B KUFUNGWA NA KUWEKWA CHINI YA SHERIA. Wagalatia 3:22-23.

- ❖ Usemi huo unaweza kueleweka kwa njia mbili tofauti:
 - Kuwa chini ya sheria kama njia mbadala ya kuupata wokovu (Wagalatia 4:21).
 - Kuwa chini ya sheria tukiwa tunahukumiwa nayo kwa sababu ya dhambi zetu (Wagalatia 3:10; Warumi 6:14-15).
- ❖ Sheria ni kama askari magereza anayemfunga yeyote aliyewahi kuivunja sheria na anakuhukumiwa kifo kwa sababu ya dhambi zake.
- ❖ Tunaweza kupata maana chanya katika maneno “kufunga” na “kufungwa”.
 - KUFUNGA: Iliyolindwa au kuhifadhiwa (Wafilipi 4:7; 1 Petro 1:5)
- ❖ KUFUNGWA: Kukusanywa, (Luka 5:6; Warumi 11:32)
- ❖ Sheria haikuwa laana bali mbaraka. Ilionesha dhambi na kumtambulisha Kristo kama njia ya wokovu (kupitia kafara). Pia iliwalinda Israeli dhidi ya vishawishi vilivyoongoza wengine katika uharibifu wa kimaadili na wa kimwili.

C SHERIA KAMA MWALIMU WETU. Wagalatia 3:24.

- ❖ Kwa nini sheria imekuwa mwalimu wetu?
 - Inafundisha na kuonesha dhambi ni nini
 - Inatuonya na kutuhukumu sisi kama wadhambi
 - Inatuongoza kwa Kristo kama njia pekee ya wokovu
- ❖ Sheria ilitolewa kuelekeza hitaji la wokovu kwa mdhambi.

D SHERIA BAADA YA IMANI. Wagalatia 3:25.

- ❖ Kristo anatuweka huru kutoka hukumu ya sheria na kuandika sheria Yake katika mioyo yetu (Waebrania 8:10). Hiyo humaanisha nini?
 - Tumesamehewa, hutuko tena chini ya hukumu ya sheria bali tuko chini ya neema (Warumi 6:14).
 - Sheria sasa imeandikwa katika mioyo yetu, Na tunaionesha tunavyoonesha tabia ya Yesu katika maisha yetu kwani sheria ni tafsiri ya tabia Yake (Tazama Mathayo 5-7).
- ❖ Tunatoaje ushirikiano kwa Mungu anapoandika sheria Yake katikati mioyo yetu??